

Aina za kware kwa madhumuni ya nyama na mayai – Coturnix, Bobwhite, California, Button, Mountain, Montezuma

Kuna aina 130 tofauti za kware ulimwenguni kote. Kuna aina bora za kware zinazofaa kufugwa shamba mwako. Kila aina hutoa kitu tofauti.

Coturnix ndiye aina bora ya kware kwa faida kadhaa. Ni aina maarufu zaidi ambayo hutoa protini. Kwa sababu ya kasi ya ukuaji wao, huwa tayari kuchinjwa wakiwa na umri wa wiki tisa. Aina hizi zinaweza kutaga mayai 100 hadi 200 kwa mwaka na kuanza kutaga wakiwa na umri wa wiki 6. Ikiwa unataka ndege kwa madhumuni ya nyama na mayai, hii ni aina bora kwako.

Aina ya bobwhite na california

Kware aina ya bobwhite ni aina bora ya kware kwa ajili ya malengo mawili. Pia hufugwa kwa ajili ya michezo. Hawakui haraka kama vile cortunix kwa hivyo hawapendekezwi kwa shughuli za kibiasara. Wanaweza kutaga mayai 200 kwa mwaka. Kware aina ya california ndio aina bora zaidi ya mapambo. Mara nyingi huhifadhiwa kwa raha nyumbani. Wao wana mwili mdogo kuliko wakilinganishwa na aina ya coturnix na bobwhite, na pia hutoa nyama na mayai kidogo sana.

Kware aina ya burton na blue scale

Kware aina ya burton wanaweza kupatikana katika maduka ya wanyama. Wana tabia kupiga mlio maalum kama vile kware wa mwituni. Wao wana mwili mdogo, na hivyo ni rahisi kuhifadhiwa kwenye banda.

Kware wa rangi ya samawati (blue scale) ndio kware bora zaidi wa kuvutia. Ni kware wa kupendeza na wa kigeni ambaye hufanya vizuri sana porini. Wao ni sigu na husafiri katika kundi. Kwa ujumla, aina ya blue scale hupatikana zaidi porini tofauti na bobwhite na coturnix.

Kware wa milimani na Montezuma

Kware wa milimani hutofautishwa na manyoya yao marefu membamba au fundo lililo juu ya vichwa vyao. Hawahifadhiwi kwa ajili ya nyama bali uzuri.

Kware wa montezuma ni hutoka nchini Mexico, na pia hujulikana kama hallequin au Menzes, na ni sura mbaya.